KANISA KATOLIKI-JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM.
PAROKIA YA MT.TERESA WA CALCUTTA-KIVULE

HISTORIA YA PAROKIA YA MT.TERESA WA CALCUTTA-KIVULE



TumsifuYesu Kristu.

Utangulizi:

Historia hii ya Parokia ya Mt. Teresa wa Culcutta Kivule imejumuisha sehemu Sita ambazo ni Historia ya Parokia, Uongozi, Changamoto,Matarajio, Mafanikio na Hitimisho.

HISTORIA YA PAROKIA

Parokia ya Mtakatifu Teresa wa Calcutta-Kivule ilitangazwa rasmi tarehe 07/07/2016 katika misa ya Upadrisho iliyofanyika Parokia ya ST Peter-Osterbay toka Parokia ya Roho Mtakatifu-Kitunda na Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo,Askofu Mkuu wa JimboKuu la Dar es Salaam,Padre Deogratias A.Chale aliteuliwa kuwa Paroko na Padre Meinrad Bigirwamungu Kalikawe aliteuliwa kuwa Paroko Msaidizi.Kwa sasa yupo Paroko peke yake anayetoahuduma Parokiani kwetu.

Safari ya kuelekea kwenye Parokia ilianza mwanzoni mwa mwaka 1986 wakati Padre Zakeo ambaye alikuwa Paroko wa Parokia ya Ukonga alipokutana na ndugu Sande Sirida na kufanya Misa ya kwanza Magole,shamba alilokuwa ana lima na mwaka huo huo walihamia kwa ndugu Adolf Kapaya na kujenga kanisa la miti ambalo walilitumia kwa miaka kumi(10).Waumini wa mwanzo walikuwa kumi na mbili(12) ambao ni Kasian Mwiya,Rusia Jakobo,Adolf Kapaya,Charles Mbwilo,Vetuda Petro,Saa Moja,Modesta Nantimbu,Patrick Riwaya,Victoria Nangadi,Antony Namandindi,Sarafina Atisa,Alphonce Basiri,Regina Adrea,Joseph Mundu,Jastini Bomola,Sixbeta Utambuli,jeradi Limwamweta,Rose Moto,Sande Sirida,Rusia Alex,Daudi Kanyaga na Erenestina Sosi.Mwaka 1987 Padre Zakeo kwa kushirikiana na waumini hao walinunua eneo hili lenye ukubwa wa ekari nane(8) kwa tshs 100,000(shilingilakimojatu) na mwaka 1997 walijenga kanisa la miti na kuzinduliwa na Mwadhama Kardinali Polycarp Pengo kikiwa kinaitwa Kigango cha MT.Teresia wa Mtoto Yesu-Magole.Tarehe 06 Januari,2016 Kigango cha MT.Theresia wa Mtoto Yesu kiliteuliwa kuwa Parokia Teule na Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo,Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar Es Salaam.







Katika kutoa huduma mbalimbali za Kiroho kama Parokia, idadi ya jumuiya ndogo ndogo za Kikristu ziliongezeka kutoka jumuiya moja ya MT.Teresia wa Mtoto Yesu na kufikia(43) arobaini na tatu kwa sasa.

Uongozi.

kwa sasa Parokia yetu inaongozwa na kamati tendaji,yenye wajumbe wafuatao:-

Aristides Rwegamba	-Mwenyekiti H/Walei
Benaford Magori	-Makamu Mwenyekiti H/Walei
Raymond P.Mmewa	-Katibu H/Walei
Amosi Hangaya	-Katibu Msaidizi H/Walei
Lilian kimoko	-Mwekahazina H/Walei
Padre Deogratias A.Chale	-Paroko

HALI YA SAKRAMENTI.

Parokia yetu imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali na kutoa sakrementi ya ndoa, ubatizo, Komunio,Kipaimara,Mpako wa wagonjwa,kitubio na kumekuwa na ongezeko kubwa la Waamini kutoa vikwazo na kuimarika kiimani.

Mafanikio:

Parokia ya Mt. Teresa wa Calcutta Kivule imepata mafanikio mengi kwa kipindi kifupi Hadi sasa Tumeanza Ujenzi za Kanisa la kudumu na tayari Msingi umekamilika na Ujenzi unaendelea. Pia tumekamilisha ujenzi wa Ukuta kuzunguka eneo lote la Kanisa pamoja na mafaniko hayo pia Yafuatayo ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana;-

i. Kupatiwa ibada ya MisaTakatifu kila dominika na siku za wiki.
ii. Kujenga kanisa la muda.
iii. Waamini wengi wamepata sakramenti mbalimbali ikiwemo ndoa, ubatizo,kipaimara,kitubio,Komunyo ya kwanza,Mpako wa wagonjwa katika Parokia.
iv. Idadi ya wakatoliki ndani ya Parokia yetu imekua ikiongezeka kwa kasi kila siku toka waumini 12 hadi 2,500 kwa sasa. Aidha tuna vyama vya kitume katika Parokia yetu ya Kivule, ambavyo ni pamoja na WAWATA, UWAKA, VIWAWA, Karismatiki Katoliki, Utoto Mtakatifu,chama cha wasomaji,watumishi wa Altare,Kolping,Legio Maria,kwaya, Moyo Mtakatifu wa Yesu.
v. Kuongezeka kwa jumuiya ndogo ndogo za kikristu,1hadi 7 mwaka 2010,toka 7 hadi 30 mwaka 2016,30 hadi 43 mwaka 2018.
vi. Kukamilika upima eneo la ekari nane la Parokia
vii. Upanuzi wa kanisa kwa kuongeza mapaa nje.
viii. Kujenga nyumba ya Mapadre wa Parokia.
ix. Ununuzi wa Gari aina ya Prado kwa ajili ya matumizi ya Parokia.
x. Ujenzi wa Sakrestia na ofisi ya Parokia.
xi. Kufanya uchanguzi kwa ngazi ya jumuiya,kanda,kigango na Parokia.
xii. Zimetolewa semina mbalimbali kwa waumini wote,vyama vya kitume na halmashauri ya Walei .
xiii. Ujenzi wa Uzio kuzunguka eneo la kiwanja kukamilika.
xiv. Kujenga na kuzindua Kigango kipya cha MT.Maria Clara-Magole.
xv. Ununuzi wa eneo jipya la kigango cha Magole

xvi. Tumeanza ujenzi wa kanisa la kudumu la Parokia kwa Hatuaya kwanza ya Msingi kukamilika.
xvii. Tumeshiriki vikao na shughuli mbalimbali ngazi ya Dekania na Jimbo.

Changamoto.

i. Mahudhurio ya wanaume kwenye ibada za jumuiya si ya kurizisha.
ii. Baadhi ya jumuiya kuwa mbali sana na eneo la Parokia,hali inayopelekea baadhi kusali makanisa mengine ya jirani.
iii. Kutokuwa na eneo la kuzikia waumini.
iv. Baadhi ya waumini wana vikwazo vya sakramenti.
v. Baadhi ya Jumuiya kutofikia malengo ya utoaji wa michango kwa wakati.

Matarajio:

Yafuatayo ni baadhi ya malengo/matarajio yetu.

i. Kukamilisha ujenzi wa kanisa la kudumu ulio anza 25 Juni 2018.
ii. Kanisa Kuendelea kuwahamasisha waamini wetu wasio na sakramenti mbalimbali waweze kupata sakramenti hizo.
iii. Kuendelea kuwa andalia mazingira mazuri waamini wetu ili waweze kuona umuhimu wa kusoma, kutafakari na kuishi kwa vitendo neno la Mungu.
iv. Kujenga ukumbi wa sherehe na mikutano, shule ya awali, msingi na sekondari katika eneo hili na kubuni miradi mingine ya kijamii itakayo wanufaisha waumini na jamii kwa ujumla.
v. Kupitia mfuko wa Vicent wa Paulo kuwasaidia waamini na watu wa medhehebu mengine wenye shida ili kuwapunguzia makali ya maisha.
vi. Ununuzi wa eneo la kuzikia waumini.
vii. Ununuzi wa pikipiki kwa ajili ya makatekista wetu.

Hitimisho:

Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwanza kwa Baba Paroko wa Parokia yetu ya Kivule kwa namna anavyojitahidi kutoa huduma Parokiani kwetu na Kigangoni na kusimamia vizuri Ujenzi wa Kanisa la Kudumu Parokia.

Hiyo ndiyo Historia ya Parokia ya MT.Teresa wa Calcutta- Kivule.

Tumsif Yesu Kristu,
Parokia ya MT.Teresa wa Calcutta-Kivule
01, Septemba, 2018.